

## Song 2 – Mama Rhoda

Artists: Jose Chameleone na Bushoke

Language Swahili

Video URL <http://www.youtube.com/watch?v=3psoHPQETeg>

### Maana ya maneno (Words and Expressions Explained)

hata- even

Kama- if

Ugenieleza- you should have told me

Kueleza- to tell

kuacha- leave

kuteseka- suffer

kutupa- forsake

utanikumbuka-You will remember me.

Nijue- I should know

Kujua- to know

Kosa- mistake

Kuliko- rather than

Peke yangu- by myself

Nafikiri- I think

kumbe- alas

unapoteza muda wangu-you are wasting my time

sikiliza- listen

nimedata- *this is a slang meaning* ( I am crazy)

unachotaka- whatever you want

ntakufata- I will follow you

njoo basi uniokoe- so come and rescue me

njoo basi unione – so come and see me

tuwe- we should be

unaniachia- you are leaving me with

unapokwenda- where you go

### Masuali (Questions)

1. Je nyimbo inahusu nini?
2. Je unafikiri mama Rhoda alikuwa anampenda mume wake? Kwanini?
3. Kwanini unafikiri mama Rhoda alimuacha mumewe? Labda.....
4. Mama Rhoda alipoondoka alimuachia baba Rhoda nani?
5. Unafikiri baada ya kuondoka mama Rhoda, jee Rhoda na baba Rhoda walikuwa na furaha? Kwanini?
6. Jee baba Rhoda anajua kosa lake?
7. Jee unafikiri mama Rhoda atarudi kwa mume wake? Kwanini?
8. Jee nini tafauti kati ya nyimbo hii na nyimbo ya Jamila?

## Mazoezi (Exercise)

1. Sikiliza nyimbo kwa makini na andika maneno ambayo yanakosekana (Listen to the song carefully and find the missing words)

### Verse 1

Hata kama ulikuwa \_\_\_\_\_ mimi \_\_\_\_\_,

\_\_\_\_\_ kuniacha mimi masikini \_\_\_\_\_

Rhoda \_\_\_\_\_ anasema \_\_\_\_\_

Na mimi \_\_\_\_\_ mama Rhoda \_\_\_\_\_

Kiitikio (chorus)

### **Mama Rhoda umeniacha Mama Rhoda utanikumbuka**

### Verse 2

Ungesema \_\_\_\_\_ langu,

Kuliko \_\_\_\_\_ hapa \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_ mingi \_\_\_\_\_ wewe wangu

Kumbe \_\_\_\_\_ muda wangu

Sikiliza

### Verse 3

Mama Rhoda \_\_\_\_\_ -

Nitakupa \_\_\_\_\_

Mwengine zaidi \_\_\_\_\_

Chameleon \_\_\_\_\_

**Kiitikio**

Mama Rhoda umeniacha  
Mama Rhoda utanikumbuka

**Verse 4**

Njoo basi \_\_\_\_\_ Bushoke \_\_\_\_\_

Njoo basi \_\_\_\_\_ Chameleon \_\_\_\_\_

**Kiitikio**

Mama Rhoda umeniacha  
Mama Rhoda utanikumbuka

**Verse 5**

Nataka \_\_\_\_\_ pamoja baby

\_\_\_\_\_ nitakupa lady

*Rhoda you drive me cracy*

\_\_\_\_\_ nani baby

**Kiitikio**

Mama Rhoda umeniacha  
Mama Rhoda utanikumbuka

\_\_\_\_\_ utanikumbuka

2. Andika kwa ufupi useme nyimbo hii inazungumzia nini?
3. Andika hadithi ya kuelezea kinachozungumzwa katika nyimbo hii.
4. Unafikiri kisa cha nyimbo hii kinaweza kutokea hapa Marekani? Kwanini?
5. Andika sentensi zenye maana kwa kutumia maneno yafuatayo:

- (i) Hata kama
- (ii) kuteseka
- (iii) kutupa
- (iv) kuliko
- (v) peke yangu
- (vi) kuokoa
- (vii) unachotaka
- (viii) kuachia

6. Soma mchezo huu wa kuigiza unaohusu nyimbo ya Mama Rhoda baadae ujibu maswali yanayofuata.

**MCHEZO: MAMA RHODA**

Waigizaji:  
Mama Rhoda  
Baba Rhoda  
Mama  
Narrator  
Jirani wa kwanza  
Jirani wa pili  
Jirani wa tatu

**Msimuliaji:** This is a story about a household where the wife wears the pants and makes all the rules. On this particular day Mama Rhoda is bossing her husband around as usual.

**Mama Rhoda:** Lazima usafishe vyombo vyote sasa hivi, na lazima uoshe hizi nguo

**Baba Roda:** Mimi ni mume wako siwezi kufanya kazi hizi!

**Mama Rhoda:** Nasema lazima ufanye!

(Mama Rhoda pushes Baba Rhoda to the floor and dumps basket of clothes on him. She then marches away, returns with Rhoda in hand and dumps the child on Baba Rhoda and leaves the home angrily)

**Baba Rhoda:** Maisha gani haya! (Rocks the crying baby and sings in an upset voice)  
Hata kama ulikuwa hunipendi mimi ungenieleza. Kuliko kuniacha mimi masikini, ninataseka. Rhoda analia, anasema umemuacha. Na mimi nimechoka kuosha vyombo na kufua nguo.

Mama Rhoda umeniacha mama Rhoda utanikumbuka \* 2

**Msimuliaji:** Mama Rhoda has fled to her mother's home and is thinking about leaving her husband for good!

**Mama Rhoda:** Hodi hodi.

**Mama:** Karibu.

**Mama Rhoda:** Shikamoo Mama?

**Mama:** Marahaba.

**Mama Rhoda:** Habari za hapa.

**Mama:** Nzuri tu. Mbona upo hapa?

**Mama Rhoda:** Mimi simpendi wala simtaki tena Baba Rhoda kwahiyo nimemuacha.

**Mama:** Nafikiri unahitaji kurudi kwasababu nasikia Rhoda analia na Baba Rhoda analia pia

**Mama Rhoda:** Lakini mama.....

**Mama:** Hapana lakini mwanangu nakwambia urudi. Haya sio maisha ya mtu kukaa peke yake.

**Mama Rhoda:** Sawa, nitarudi

**Msimuliaji:** Meanwhile back at the home of Mama and Baba Rhoda some of their neighbors walk by and notice Baba Rhoda doing chores and tending to the baby.

**Jirani wa kwanza:** Baba Rhoda kwanini unafanya kazi za nyumba?

**Nirani wa pili:** Ndio, mkeo yuko wapi?!

**Baba Rhoda:** (Sadly) Mke wangu ameniacha.

**Jirani wa tatu:** Tokea lini mwanamke kumuacha mwanamme? Baba Rhoda wewe ni dhaifu sana.

(The three neighbors walk away pointing, shaking their head in disbelief and laughing at Baba Rhoda)

**Msimuliaji:** Mama Rhoda has decided to take her mother's advice and return to her husband and child.

**Mama Rhoda:** Basi mama mimi ninarudi kwa mume wangu.

**Mama:** Sawa. Vizuri mwanangu.

**Mama Rhoda:** Kwaheri mama.

**Mama:** Sawa kwaheri mwanangu.

**Mama Rhoda:** Nimekukumbuka mume wangu.

**Baba Rhoda:** Nimekusamehe mke wangu na Rhoda pia amekusamehe.

## MWISHO

Masuali

1. Mama Rhoda anamtaka mume wake afanye nini?
2. Mama Rhoda anafanya nini baada ya kumuacha mume wake nyumbani?
3. Jee mama yake mama Rhoda anatoa ushauri gani baada ya mwanawe kumuacha mumewe?
4. Jee mama Rhoda anasikiliza ushauri wa mama yake?
5. Jee unafikiri ni kwanini majirani wanashangaa wanapomuona baba Rhoda anafanya kazi za nyumbani?

6. Jee watu wa Marekani wanaweza kushangaa wanaposikia kuwa mwanamke kamuacha mume wake? Elezea.
7. Jee kisa kama hiki kinaweza kutokea hapa Marekani? Kinaweza kutokea vipi? Una mfano wowote?